JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS



TUME YA UTUMISHI WA UMMA

HOTUBA YA MHE. JENISTA J. MHAGAMA (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

WAKATI WA UZINDUZI WA TUME YA UTUMISHI WA UMMA ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA OFISI ZA TUME YA TAIFA UCHAGUZI – DODOMA, TAREHE 23 MEI, 2022

HOTUBA YA MHE. JENISTA J. MHAGAMA (MB.), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA WAKATI WA UZINDUZI WA TUME YA UTUMISHI WA UMMA ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA OFISI ZA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI – DODOMA, TAREHE 23 MEI, 2022

Mhe. Deogratius J. Ndejembi (Mb.), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

Mhe. Jaji (Mst.) Hamisa Hamis Kalombola, Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma;

Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Umma;
Mhe. Balozi John M. Haule,
Mhe. Immaculate P. Ngwale,
Mhe. Khadija A. M. Mbarak,
Mhe. Balozi Adadi M. Rajabu,
Mhe. Susan P. Mlawi,
Mhe. Nassor N. Mnambila;

Dkt. Laurean J.P Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

Bw. Xavier M. Daudi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

Bw. Mathew M. Kirama, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma;

Wakuu wa Idara na Vitengo wa Tume ya Utumishi wa Umma;

Waandishi wa Habari;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana;

Ninawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nguvu na afya ya kuweza kutukutanisha hapa leo kwenye uzinduzi wa Tume ya Utumishi wa Umma ambao utaenda sambamba na mafunzo elekezi kwa Makamishna Wateule wa Tume hii. Pili, nichukue fursa hii kukupongeza wewe Mwenyekiti pamoja na Makamishna wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuiongoza Tume hii kwa kipindi cha miaka mitatu. **Hongereni sana.**

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Mheshimiwa Rais amefanya uteuzi wenu kwa umakini mkubwa na kwa kuzingatia wasifu wa kila mmoja wenu. Hii inadhihirisha kuwa Mheshimiwa Rais ana imani kubwa kuwa

mtatekeleza vema jukumu hili muhimu. Ninafahamu kuwa miongoni mwenu, wapo Makamishna ambao walikuwepo kwenye Tume hii katika kipindi kilichopita na walitekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi mkubwa. Ni kwa kutambua mchango wenu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amewateua kwa kipindi kingine tena ili muendelee kutekeleza jukumu hili la kusimamia haki za Watumishi wa Umma, Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu. Niwasihi mtumie uzoefu mlioupata katika kipindi cha miaka mitatu mliyotumikia Tume kuendelea kutekeleza jukumu hili na kubadilishana uzoefu huo na Makamishna wenzenu ambao wameteuliwa kwenye Tume hii kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Naishukuru pia Sekretarieti ya Tume yako kwa kunialika kuja kuzindua Tume hii na baadaye mafunzo elekezi kwenu ambayo yameandaliwa mahsusi kwa ajili ya kuwajengea uwezo ili muweze kutekeleza kwa ufanisi jukumu hili muhimu mlilokabidhiwa.

Kwa namna ya pekee niwapongeze waandaaji wa shughuli hii ya uzinduzi wa Tume pamoja na mafunzo haya ambayo yatajenga uelewa wa pamoja wa majukumu yenu katika Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Jukumu kubwa la Tume ya Utumishi wa Umma ni kuhakikisha kwamba usimamizi na uendeshaji wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma unatekelezwa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma. Ili kuhakikisha kuwa mnasimamia kwa ukamilifu jukumu hili, nimeelezwa kuwa, baada ya uzinduzi wa Tume yetu, mtakuwa na mafunzo elekezi ya siku tatu. Katika mafunzo hayo, mada saba (7) zitawasilishwa na Wawezeshaji kutoka Ofisi ya Rais – Ikulu, Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Umma nanyi mtapata fursa ya kuzijadili na kubadilishana uzoefu. Mada hizo ni pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 na marekebisho yake; Ushughulikiaji wa Mashauri ya Nidhamu katika Utumishi wa Umma; Uchambuzi wa Rufaa na Malalamiko; Mambo ya kuzingatia wakati wa Ushughulikiaji wa Rufaa na Malalamiko; Uzoefu wa Ofisi ya Rais - Ikulu katika

Ushughulikiaji wa Rufaa na Malalamiko ya Watumishi wa Umma; Jukumu la Urekebu la Tume ya Utumishi wa Umma na Usalama wa Nyaraka na Usiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Ni imani yangu kuwa baada ya mawasilisho ya mada hizi, mtakuwa mmeongeza uelewa wa namna ya kutekeleza majukumu yaliyo mbele yenu kwani sote tunafahamu kuwa Rasilimali Watu ndiyo rasilimali muhimu kuliko rasilimali zote kwa kuwa rasilimali hii ndiyo inayozisimamia rasilimali nyingine zote. Hivyo, Rasilimali Watu ikisimamiwa kikamilifu, Utumishi wa Umma utakuwa wenye matokeo na tija kwa Taifa letu na tutakuwa tumeunga mkono jitihada za Serikali yetu ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuhakikisha kwamba Utumishi wa Umma unaendelea kuwa injini ya maendeleo ya nchi yetu na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Nina hakika kuwa kwa sasa Tume inazo Rufaa na Malalamiko mengi ambayo yanawasubiri kwa ajili ya

kuyatolea uamuzi. Nitoe rai kwenu mjitahidi kuzishughulikia na kuzikamilisha ili tuweze kutenda haki na kuondoa sintofahamu kwa Warufani ambao wanasubiri majibu ya rufaa zao kutoka Tume. Tukumbuke kuwa, uongozi makini ni pamoja na kuzingatia uzalendo, uaminifu na kutenda haki. Tusipofanya uamuzi sahihi na kwa wakati, tutaongeza malalamiko katika Utumishi wa Umma na kukwamisha shughuli za maendeleo na huduma muhimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Ninafahamu kuwa Tume inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo baadhi ya Mamlaka za Nidhamu kuchelewa kuwasilisha vielelezo vya rufaa zilizokatwa Tume; kutokuwa na jengo la Ofisi pamoja na ukomo mdogo wa bajeti. Niwahakikishie kuwa, kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Tume, Wizara yangu itaendelea kuchukua hatua kadhaa ili kutatua changamoto hizi. Aidha, nikuhakikishie Mheshimiwa Mwenyekiti na Makamishna wa Tume kwamba Ofisi yangu itakuwa tayari wakati wote mtakapohitaji kuishirikisha katika suala lolote linalohusiana na namna ya kuboresha utendaji wa Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Viongozi mliopo,

Katika kutatua changamoto ya ucheleweshwaji wa vielelezo vya rufaa, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inafanya marekebisho ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Marekebisho hayo yataipa Tume mamlaka ya kusikiliza na kuamua rufaa kwa kutumia vielelezo vya upande mmoja endapo upande mwingine utashindwa kuwasilisha nyaraka zinazohitajika kwa wakati.

Aidha, wakati Kanuni hizi zinafanyiwa marekebisho, nitoe agizo kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu ambazo hazijawasilisha vielelezo vya rufaa na malalamiko vilivyoombwa na Tume, kuhakikisha kuwa zinawasilisha mara moja vielelezo hivyo ili kuiwezesha Tume kushughulikia mashauri husika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Nilipata fursa ya kuhitimisha zoezi la Ukaguzi wa Rasilimali Watu lililoendeshwa na Tume tarehe 02 Aprili, 2022, hivyo, ninafahamu kuwa Tume inatekeleza majukumu muhimu sana ambayo kimsingi yanashabihiana na yale ya Mdhibiti

na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG). Wakati Tume inakagua usimamizi wa Rasilimali Watu, CAG anakagua usimamizi wa mapato na matumizi ya Rasilimali Fedha. Kama nilivyoeleza awali, kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Tume tumeshaanza kuchukua hatua kuhakikisha kuwa Tume inakuwa na mazingira mazuri yatakayoiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa ajili ya ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wa Umma ambao wataonekana kukiuka Sheria kwa kufanya kazi bila kuzingatia maadili ya Utumishi wa Umma na ya Taaluma zao. Nitoe rai kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu pamoja na Watumishi wote wa Umma wahakikishe kuwa wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma. Kwa kufanya hivyo, Watumishi wa Umma watajiepusha na kuchukuliwa hatua za kinidhamu na hivyo kulinda na kuendeleza utumishi wao ambao unahitajika kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Kwa upande mwingine, Mamlaka za Ajira na Nidhamu zinapaswa kujiridhisha kama kuna ukiukwaji wa Sheria na Kanuni uliofanyika kabla ya kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wa Umma ili kuepuka kuchukua hatua kwa uonevu na kuisababishia Serikali hasara kwa kuendesha mashauri ya kinidhamu yasiyo na mashiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Nikiwa Waziri Mwenye Dhamana ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, niwasihi Makamishna wa Tume hii kuhakikisha kuwa kila mtakapopata fursa ya kukutana na Waajiri, Mamlaka za Ajira, Mamlaka za Nidhamu na Watumishi wa Umma wakati wa ziara zenu, muwaelimishe na kuwakumbusha kuhusu kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma. Mkakati wa Tume wa kuelimisha wadau wake ukitekelezwa vizuri, utasaidia kupunguza vitendo vya ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti;

Baada ya kusema haya, kwa mara nyingine tena, natoa pongezi zangu nyingi kwenu kwa kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Umma na ninatamka kuwa Tume hii imezinduliwa rasmi. Aidha, nichukue fursa hii kutamka kuwa mafunzo elekezi mtakayoyaanza hivi punde yamefunguliwa rasmi. Nawatakia mafunzo mema na utekelezaji mwema wa majukumu yenu yajayo.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA